

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

Anuani ya Simu: "TAMISEMI"
Simu Na: (026) 2322848, 2321607
2322853, 2322420
Nukushi: (026) 2322116, 2322146
2321013

Barua pepe: ps@pmoralg.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:



Tawala za Mikoa na
Serikali za Mitaa,
S.L.P. 1923,
DODOMA.

Kumb. Na. AB.13/68/01/67

05 Novemba, 2014

Makatibu Tawala wa Mikoa
Tanzania Bara

Yah: MWONGOZO WA UUNDAJI WA KAMATI ZA KUDHIBITI UKIMWI
KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

Tafadhali rejeeni somo tajwa hapo juu.

1. Kwa zaidi ya miaka thelathini Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikitekeleza afua mbalimbali za mwitikio wa kitaifa dhidi ya VVU na UKIMWI katika jamii. Mwaka 2003 uliandaliwa Mwongozo wa Uundaji wa Kamati za Kudhibiti UKIMWI katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzia ngazi ya Kitongoji, Kijiji, Mtaa, Kata, Mji Mdogo, Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji. Lengo mahsusi la mwongozo huu ulikuwa ni kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuchukua jukumu muhimu la mwitikio dhidi ya VVU na UKIMWI.
2. Mwongozo wa Kamati za Kudhibiti UKIMWI wa mwaka 2003 umetumika kwa zaidi ya miaka kumi (10) sasa hivyo kutoendana na hali halisi ikizingatiwa mabadiliko yaliyotokea katika Sera, Sheria, Mikakati mbalimbali, maendeleo ya ugonjwa wenyewe na huduma zake.
3. OWM-TAMISEMI kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania imehuisha mwongozo uliotolewa mwaka 2003 ili kukidhi mahitaji ya sasa.

4. Mwongozo huu mpya umembatishwa na barua hii ili usambazwe kwenye Halmashauri zilizo chini yenu. Kila Mkurugenzi wa Halmashauri na Afisa anayehusika katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI anapaswa kutekeleza maelekezo yote yaliyomo katika mwongozo huu.
5. Hivyo kwa barua hii, mnatakiwa kuhakikisha kuwa Wakurugenzi wa Halmashauri zilizo chini ya Mamlaka zenu wanapata Mwongozo huu na wanatekeleza ipasavyo.

Ni matumaini yetu kuwa mtalipa uzito unaostahili suala hili kwa manufaa ya taifa letu.

Nawatakia utekelezaji mwema.


J.A. Sagini
KATIBU MKUU

Nakala: Katibu Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu,
S.L.P 3021,
DAR ES SALAAM.

Mwenyekiti Mtendaji,
Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania,
S.L.P 76987,
DAR ES SALAAM.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



**OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MWONGOZO WA UUNDAJI WA KAMATI ZA KUDHIBITI
UKIMWI KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA**

Umetolewa na:

**OWM-TAMISEMI,
S.L.P 1923,
DODOMA.**

Simu Na: (026) 2322848, 2321607
2322853, 2322420

Nukushi: (026) 2322116, 2322146
2321013

Barua pepe: ps@pmoralg.go.tz

NOVEMBA, 2014

MWONGOZO WA UUNDAJI WA KAMATI ZA KUDHIBITI UKIMWI KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

1.0 UTANGULIZI

Kwa zaidi ya miaka thelathini Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikitekeleza afua mbalimbali za mwitikio wa kitaifa dhidi ya VVU na UKIMWI katika jamii. Miongoni mwa juhudi hizo ni uundaji wa Sera, Mikakati, Sheria na Miongozo mbalimbali.

Mwaka 2003 uliandaliwa mwongozo wa uundaji wa Kamati za Kudhibiti UKIMWI katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzia ngazi ya Kitongoji, Kijiji, Mtaa, Kata, Mji Mdogo, Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji. Mwongozo huu uliandaliwa kwa kuzingatia Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura Namba 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura Namba 288 toleo la 2002 pamoja na sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ya mwaka 2001. Lengo mahsusi la mwongozo huu ni kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuchukua jukumu muhimu la mwitikio dhidi ya VVU na UKIMWI.

Mwongozo wa Kamati za Kudhibiti UKIMWI uliotolewa mwaka 2003 umetumika kwa zaidi ya miaka kumi (10) sasa hivyo kutoendana na hali halisi ikizingatiwa mabadiliko yaliyotokea katika Sera, Sheria na Mikakati mbalimbali, maendeleo ya ugonjwa wenyewe na huduma zake. Aidha mabadiliko katika mifumo ya maisha ya jamii, tabia na mienendo vinavyochangia maambukizo ya VVU na athari zake kama vile kupata UKIMWI.

Vilevile, mapitio ya Mwongozo wa Kamati za Kudhibiti UKIMWI ulifanyika kufuatia matokeo ya tafiti zilizofanyika katika kupima ufanisi wa utendaji wa kamati hizi, tafiti zilionesha upungufu katika Muundo, Uteuzi na Sifa za Wajumbe na Wakaribishwa, Ukomo wa Ujumbe, Wajibu wa Wajumbe, Uwezeshaji wa Kamati na Sifa na Uteuzi wa Waratibu wa UKIMWI. Tafiti

zimeonyesha kuwapo na changamoto nyingi hususani ngazi ya vitongoji, Vijiji/mitaa na kata kwa kutotekeleza majukumu yao kama ilivyokusudiwa.

Mchakato wa mapitio ya mwongozo wa Kamati za Kudhibiti UKIMWI umeshirikisha Watendaji wa Kata, Vijiji na Mitaa; Wawakilishi wa vijana, Wizara ya Afya (Kitengo cha Ustawi wa Jamii), Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto, Umoja wa Mameya wanaoshughulika na UKIMWI (AMICAALL), Asasi zisizo za kiserikali za SIKIKA na Baraza la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (NACOPHA), Waratibu wa UKIMWI wa Halmashauri, Waratibu wa UKIMWI Sekta ya Afya, Waratibu wa UKIMWI wa Mikoa, Waratibu wa UKIMWI wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Wakurugenzi wa Halmashauri.

Aidha, rasimu ya mwongozo wa kamati za kudhibiti UKIMWI uliwasilishwa katika mkutano wa 30 wa Jumuiya ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania (ALAT) mwezi Mei 2014 na baadaye rasimu hiyo ilipitishwa katika kongamano la wiki ya Serikali za Mitaa lililofanyika Jijini Tanga tarehe 28 Juni, 2014.

Lengo la waraka huu ni kuhuisha mwongozo uliotolewa mwaka 2003 na mwongozo huu uanze kutumika katika kuhakikisha kamati zinaundwa mahali ambapo kamati hazijaundwa na kuboresha kamati zilizopo sasa kwa kufuata maelekezo ya waraka huu.

2.0 MUUNDO WA KAMATI

2.1. Ngazi ya Halmashauri ya Jiji, Manispaa, Miji, Wilaya na Mamlaka ya Mji Mdogo

Katika ngazi ya Halmashauri ya Jiji isipokuwa Dar es Salaam, Kamati hizi zitajulikana kama "Kamati ya Kudhibiti UKIMWI ya Halmashauri ya Jiji, Manispaa, Miji, Wilaya na Mamlaka ya Mji Mdogo.

2.1.1 Muundo wa Kamati

Kamati itakuwa na wajumbe wafuatao:-

Wajumbe wa Kamati:

- | | | |
|------------|---|---|
| Mwenyekiti | - | Naibu Meya/Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri |
| Katibu | - | Mkurugenzi wa Halmashauri |
| Wajumbe | - | Waheshimiwa Wabunge wote wa kuchaguliwa na kuteuliwa kutoka kwenye Majimbo yaliyomo ndani ya Halmashauri. |
| | - | Waheshimiwa Madiwani 4 ikiwa wawili (2) wa kuchaguliwa na wawili (2) wa kuteuliwa kwa kuzingatia jinsi |
| | - | Mstahiki Meya/Mwenyekiti wa Halmashauri |

Wakaribishwa:

- a) Wawakilishi 2 (Me na Ke) wa Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) kutoka kwenye Konga.
- b) Wawakilishi 2 wa Viongozi wa madhehebu ya dini ya Kiislamu na Kikristo.
- c) Mwakilishi 1 wa mtandao wa Asasi zisizo za kiserikali zinazoshughulika na afua za VVU na UKIMWI.
- d) Wawakilishi 2 wa vijana (Me na Ke) kutoka katika mtandao wa vijana.
- e) Wawakilishi 2 (Me na Ke) wa watu wenye mahitaji maalum kutoka katika Shirikisho la vyama vya watu wenye ulemavu.
- f) Wawakilishi 2 kutoka Baraza la Wazee la Halmashauri.

NB: Mwakilishi wa dini nyingine kama zipo kadiri Halmashauri itakavyoona inafaa.

Wataalam:

- a) Mratibu wa UKIMWI wa Halmashauri (CHAC)
- b) Mratibu wa UKIMWI Sekta ya Afya (DACC)
- c) Afisa Maendeleo ya Jamii
- d) Mganga Mkuu wa Halmashauri
- e) Afisa Utumishi wa Halmashauri
- f) Afisa Elimu - Msingi
- g) Afisa Elimu - Sekondari
- h) Afisa Utamaduni
- i) Afisa Ustawi wa Jamii
- j) Afisa Dawati la Jinsia Polisi
- k) Afisa Mipango

Endapo itahitajika kumwalika mgeni au mtaalamu yeyote Katibu atamwalika kwa kushauriana na Mwenyekiti.

2.1.2 Wajibu na Majukumu ya Kamati ya Halmashauri

Wajibu na Majukumu ya Kamati yatakuwa kama ifuatavyo:-

- a) Kuhakikisha kamati za VVU na UKIMWI zinaundwa na kufanya kazi kwa kila ngazi kwa kufuata miongozo inayotolewa.
- b) Kuhakikisha tathmini ya hali halisi ya VVU na UKIMWI katika Halmashauri inafanyika na kuweka mikakati ya utekelezaji kila mwaka.
- c) Kuhakikisha mipango yote ya UKIMWI na wadau wanaotelekeza katika Halmashauri husika vinaingizwa kwenye Mpango Mkakati wa UKIMWI wa Halmashauri na Mkoa ili kuondoa urudufu wa juhudi na rasilimali.
- d) Kuhimiza Halmashauri kutenga fedha za mapato ya ndani na kushirikisha wadau katika kuchangia rasilimali hizo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kudhibiti UKIMWI.

- e) Kuhakikisha uwepo wa orodha hai ya Wadau wa masuala ya UKIMWI katika Halmashauri.
- f) Kutoa ushauri kwa ngazi inayohusika kuhusu Sera au Sheria ndogo juu ya udhibiti wa VVU na UKIMWI.
- g) Kuhakikisha Sera, Mkakati wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI, Sheria, Miongozo na matokeo ya tafiti mbalimbali ya masuala ya UKIMWI yanawafikia wadau na wananchi kwa ujumla.
- h) Kutambua na kutathmini shughuli za wadau mbalimbali wanaotekeleza afua za VVU na UKIMWI katika Halmashauri.
- i) Kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za VVU na UKIMWI zilizopangwa.
- j) Kupitia taarifa za uratibu zinazofanywa na Halmashauri na kutoa ushauri wa namna ya kuimarisha na kuongeza ufanisi.
- k) Kutoa taarifa ya shughuli za VVU na UKIMWI kwenye Baraza la Madiwani kila baada ya miezi mitatu.

2.2 Ngazi ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam

2.2.1. Muundo wa Kamati

Muundo wa kamati katika ngazi ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Jiji lingine lolote litakalo kuwa na muundo kama wa Jiji la Dar es Salaam; kamati hii itajulikana kama “Kamati ya Kudhibiti UKIMWI ya Halmashauri ya Jiji” ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

Wajumbe wa Kamati:

- | | | |
|------------|---|--|
| Mwenyekiti | - | Mstahiki Meya |
| Katibu | - | Mkurugenzi wa Jiji |
| Wajumbe | - | Manaibu Mameya/ Makamu Wenyeviti wa Halmashauri zote |
| | - | Mameya wa Manispaa zote za jiji |

Wakaribishwa - Wataalamu

- a) Afisa Utumishi wa Jiji la Dar es Salaam
- b) Mratibu wa UKIMWI [Afya] kutoka Manispaa zote za jiji
- c) Mratibu wa UKIMWI [Jamii] kutoka Manispaa zote za jiji

2.2.2. Majukumu ya Kamati:

Kamati hii kimsingi ni kiungo kati ya Kamati za Kudhibiti UKIMWI za Manispaa za Jiji la Dar es Salaamu na Sekretaireti ya Mkoa wa DSM.

Wajibu na majukumu ya kamati:-

- a) Kuratibu na Kutoa Ushauri kuhusu shughuli za UKIMWI katika Jiji la Dar es Salaam zilizo Mtambuka kwa Manispaa zote ikiwemo matumizi ya sheria ndogo;
- b) Kuratibu afua za UKIMWI mahali pa kazi kwa watumishi wa Jiji.
- c) Kupokea nakala za taarifa za kamati shirikishi za Manispaa zote (kwa taarifa) na kushauri
- d) Kushiriki katika maadhimisho yanayohusu shughuli za UKIMWI zinazofanyika Jijini Dar es Salaam.

2.3 Ngazi ya Kata

2.3.1 Muundo wa Kamati

Katika ngazi ya Kata kamati hii itajulikana kama "Kamati ya Kata ya Kudhibiti UKIMWI" ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao;

Wajumbe wa Kamati:

- | | | |
|----------------|---|------------------------|
| (a) Mwenyekiti | - | Mheshimiwa Diwani |
| (b) Katibu | - | Afisa Mtendaji wa Kata |

- (c) $\frac{1}{3}$ ya wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kata kwa kuzingatia uwiano wa kijinsi.

Wakaribishwa

- a) Wawakilishi 2 wa madhehebu ya dini (1 Kiislamu na 1 Kikristo.
- b) Wawakilishi 2 (Me na Ke) wa Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) kutoka katika vikundi vya WAVIU.
- c) Mwakilishi 1 wa mtandao wa Asasi zisizo za Kiserikali zinazoshughulika na afua za VVU na UKIMWI zilizoko kwenye Kata husika.
- d) Mwakilishi 1 mtoa huduma za wagonjwa nyumbani.
- e) Wawakilishi 2 (Me na Ke) wa Sekta binafsi isiyo rasmi
- f) Wawakilishi 2 wa vijana (Me na Ke) kutoka katika mtandao/mitandao wa vijana.
- g) Wawakilishi 2 (Me na Ke) wa Baraza la Wazee la Kata

NB: Mwakilishi wa dini nyingine kadiri Kata itakavyoona inafaa.

Wataalam

- a) Afisa Maendeleo ya Jamii
- b) Walimu 2 wa Sekondari (Me na Ke)
- c) Walimu 2 wa Msingi (Me na Ke)
- d) Mganga Mfawidhi wa Zahanati/Kituo cha afya
- e) Mratibu Elimu Kata
- f) Afisa Ustawi wa Jamii
- g) Maafisa ugani walio kwenye Kata

2.3.2 Wajibu na Majukumu ya Kamati

- a) Kutafuta vyanzo vya mapato kutoka kwa wadau mbalimbali ili kuongeza rasilimali katika utekelezaji wa shughuli za VVU na UKIMWI katika Kata.

- b) Kutambua vichocheo vya maambukizo ya VVU katika Kata na kuweka mkakati wa kudhibiti.
- c) Kutathmini hali halisi ya VVU na UKIMWI katika Kata.
- d) Kutambua na Kutathmini shughuli za wadau mbalimbali katika Kata.
- e) Kuratibu mipango ya VVU na UKIMWI kutoka ngazi ya Vijiji na Mitaa.
- f) Kutoa ushauri kwa ngazi inayohusika kuhusu Sera au sheria ndogo juu ya udhibiti wa VVU na UKIMWI.
- g) Kuhakikisha Sera, Mkakati wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI, Sheria, Miongozo na matokeo ya Tafiti mbalimbali wa masuala ya UKIMWI vinawafikia wadau na wananchi kwa ujumla.
- h) Kuhakikisha Kamati za Kudhibiti UKIMWI ngazi Mtaa/Kijiji zinaundwa na kufanya kazi kwa kufuata utaratibu, Miongozo na Sheria zilizopo.
- i) Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Kamati za kudhibiti UKIMWI za Mitaa na Vijiji.
- j) Kutoa taarifa ya shughuli za VVU na UKIMWI kwa Kamati ya Maendeleo ya Kata na Kamati ya UKIMWI ya Halmashauri kila robo mwaka.
- k) Kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.
- l) Kuhakikisha uwepo wa orodha ya wadau wanaoshughulika na afua za VVU na UKIMWI katika Kata.
- m) Kuhakikisha uwepo wa takwimu za WAVIU, Wajane, Watoto Wanaoishi Katika Mazingira Hatarishi, Wagonjwa wa majumbani, Walemavu na Wazee.
- n) Kutunza na kuhuisha takwimu zinazohusu VVU, UKIMWI na athari zake kwenye Daftari la Kata.

- o) Kuunganisha mipango ya UKIMWI kutoka Vijiji /Mitaa na kuwasilisha katika ngazi ya Halmashauri kupitia zana ya uandaaji Mpango Mkakati wa VVU na UKIMWI wa Mkoa.

2.4 Ngazi ya Halmashauri ya Kijiji

2.4.1 Muundo wa Kamati

Katika ngazi ya Halmashauri ya kijiji, iundwe Kamati itakayojulikana kama "Kamati maalumu ya Kudhibiti UKIMWI " ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

Wajumbe wa Kamati:

- a) Mwenyekiti - Mwenyekiti wa Kijiji
- b) Katibu - Afisa Mtendaji wa Kijiji
- c) $\frac{1}{3}$ ya Wajumbe kutoka Halmashauri ya kijiji kwa kuzingatia uwiano wa kijinsi.

Wakaribishwa

- a) Wawakilishi 2 wa madhehebu ya dini ya Kiislamu na Kikristu yaliyo katika kijiji.
- b) Wawakilishi 2 wa vijana (Me na Ke) watakaopatikana kupitia mitandao ya vijana ndani ya Kijiji.
- c) Wawakilishi 2 wa Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) (Me na Ke) watakaopatikana kupitia vikundi vya WAVIU ndani ya Kijiji.
- d) Watu wawili (Me na Ke) wenye kuleta msukumo/walio mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI ndani ya kijiji.
- e) Mwakilishi wa watoa huduma za wagonjwa nyumbani.
- f) Mwakilishi 1 wa Asasi za kiraia zinazoshughulika na UKIMWI ngazi ya Kijiji.

- g) Wawakilishi 2 (Me na Ke) wa Sekta binafsi isiyo rasmi.
- h) Mwakilishi wa kamati ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

NB: Mwakilishi wa dini nyingine kadiri Serikali ya Kijiji itakavyoona inafaa.

Wataalam

- a) Walimu 2 wa shule za Sekondari (Me na Ke) watoke ngazi ya Kata
- b) Walimu 2 wa shule za Msingi (Me na Ke)
- c) Mganga Mfawidhi wa Zahanati /Kituo cha afya kilichopo ndani ya Kijiji.

2.4.2 Wajibu na Majukumu ya Kamati

- a) Kutathmini hali halisi ya VVU na UKIMWI katika kijiji na kuweka mkakati wa utekelezaji.
- b) Kutambua na kujadili vichocheo vya maambukizo ya VVU katika kijiji ikiwa ni pamoja na vile vinavyotokana na utumiaji wa madawa ya kulevya, biashara ya ngono, ngono za kinyume na maumbile na kuweka mikakati ya udhibiti wa hali hiyo.
- c) Kukusanya takwimu mbalimbali za watu wanaoishi na VVU, Wajane, Watoto Wanaoishi Katika Mazingira Hatarishi na Wagonjwa wa majumbani.
- d) Kuandaa mpango wa mwaka wa afua ya UKIMWI kwa kushirikiana na wananchi na wadau wengine na kuwezesha makundi yenye mahitaji maalumu (WAVIU, Wajane, Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi).
- e) Kuhimiza Serikali ya kijiji kutenga fedha na kushirikisha wadau mbalimbali katika kuchangia rasilimali hizo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kudhibiti UKIMWI.

- f) Kuratibu afua za UKIMWI zinazotekelezwa na wadau kulingana na vipaumbele vya kijiji.
- g) Kuhakikisha uwepo wa orodha hai ya wadau wa masuala la UKIMWI katika kijiji.
- h) Kutoa ushauri kwa ngazi inayohusika kuhusu Sera au Sheria ndogo juu ya udhibiti wa VVU na UKIMWI.
- i) Kuhakikisha Sera, Mkakati wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI, Sheria, Miongozo na matokeo ya Tafiti mbalimbali wa masuala ya UKIMWI vinawafikia wadau na wananchi kwa ujumla.
- j) Kutoa taarifa ya shughuli za VVU na UKIMWI kwenye Serikali ya kijiji na Kamati ya Maendeleo ya Kata kila baada ya miezi 3.
- k) Kutunza na kuhuisha takwimu zinazohusu VVU, UKIMWI na athari zake kwenye daftari la kijiji.

2.5 Ngazi ya Mtaa

2.5.1 Muundo wa Kamati

Katika ngazi ya Halmashauri ya mtaa Kamati itajulikana kama “Kamati ya Mtaa ya Kudhibiti UKIMWI” ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

Wajumbe wa Kamati:

- a) Mwenyekiti - Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa
- b) Katibu - Afisa Mtendaji wa Mtaa.
- c) $\frac{1}{3}$ ya Wajumbe kutoka Serikali ya Mtaa kwa kuzingatia jinsi.

Wakaribishwa

- a) Wawakilishi 2 wa madhehebu ya dini ya Kikristu na Kiislamu yaliyo katika Mtaa husika.

- b) Wawakilishi 2 wa vijana (Me na Ke) watakaopatikana kupitia mitandao ya Vijana ndani ya Mtaa husika.
- c) Wawakilishi 2 wa WAVIU (Me na Ke) watakaopatikana kupitia vikundi vya WAVIU ndani ya Mtaa husika.
- d) Watu 2 wenye kuleta msukumo/walio mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI ndani ya jamii husika (Me na Ke).
- e) Mwakilishi wa mtoa huduma za wagonjwa nyumbani.
- f) Mwakilishi 1 wa Asasi za kiraia zinazoshughulika na UKIMWI.

Wataalam

- a) Maafisa Ugani wote wanaopatikana kwenye Mtaa.
- b) Mganga Mfawadhi wa Zahanati/kituo cha afya kilichopo ndani ya mtaa.
- c) Walimu 2 wa shule za Sekondari (Me na Ke) kutoka eneo la Mtaa/ Kata.
- d) Walimu 2 wa shule za Msingi (Me na Ke) kutoka eneo la Mtaa.

2.5.2 Wajibu na Majukumu ya Kamati

- a) Kutathmini hali halisi ya VVU na UKIMWI katika Mtaa na kuweka mkakati wa utekelezaji.
- b) Kutambua na kujadili vichocheo vya maambukizo ya VVU katika mtaa ikiwa ni pamoja na vile vinavyotokana na utumiaji wa madawa ya kulevya, biashara ya ngono, ngono za kinyume na maumbile na kuweka mikakati ya udhibiti wa hali hiyo.
- c) Kukusanya takwimu mbalimbali za watu wanaoishi na VVU, Wajane, Watoto Wanaoishi Katika Mazingira Hatarishi na Wagonjwa wa majumbani.

- d) Kuandaa mpango wa mwaka wa afua ya UKIMWI kwa kushirikiana na wananchi na wadau wengine na kuwezesha makundi yenye mahitaji maalumu (WAVIU, Wajane, Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi).
- e) Kuhimiza Serikali ya Mtaa kutenga fedha na kushirikisha wadau mbalimbali katika kuchangia rasilimali hizo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kudhibiti UKIMWI.
- f) Kuratibu afua za UKIMWI zinazotekelezwa na wadau kulingana vipaumbele vya mtaa.
- g) Kuhakikisha uwepo wa orodha hai ya wadau wa masuala la UKIMWI katika Mtaa.
- h) Kutoa ushauri kwa ngazi inayohusika kuhusu Sera au Sheria ndogo juu ya udhibiti wa VVU na UKIMWI.
- i) Kuhakikisha Sera, Mkakati wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI, Sheria, Miongozo na matokeo ya Tafiti mbalimbali wa masuala ya UKIMWI vinawafikia wadau na wananchi kwa ujumla.
- j) Kutoa taarifa ya shughuli za VVU na UKIMWI kwenye Serikali ya Mtaa na Kamatiya Maendeleo ya Kata kila baada ya miezi 3.
- k) Kutunza na kuhuisha takwimu zinazohusu VVU, UKIMWI na athari zake kwenye daftari la mtaa.

3.0 UUNDAJI WA KAMATI

3.1 Mambo ya kuzingatia wakati wa Uundaji wa Kamati

Wajumbe wa Kamati watachaguliwa kwa kuzingatia utaratibu wa uundaji wa Kamati za Mamlaka za Serikali za Mitaa baada ya Uchaguzi Mkuu.

3.2 Uteuzi wa Wakaribishwa

Uteuzi wa Wakaribishwa utafanyika kwa utaratibu ufuatao:-

- i. **Taasisi zilizo Rasmi:** Asasi za Kiraia (AZAKI) na Madhehebu ya Dini
Mkurugenzi wa Halmashauri/ Afisa Mtendaji wa ngazi husika ataziandikia barua taasisi/mitandao iliyotajwa hapo juu ili wafanye uteuzi kwa kuzingatia sifa zilizoanishwa katika mwongozo huu.
- ii. Vikundi vya Jamii, Vijana na Watu wanaoishi na VVU (WAVIU)
 - a. Mkurugenzi wa Halmashauri/ Afisa Mtendaji wa ngazi husika awezeshe mchakato wa upatikanaji wa mwakilishi wa vijana (Me na Ke) kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa kwenye mwongozo huu.
 - b. Mkurugenzi wa Halmashauri/ Afisa Mtendaji wa ngazi husika awezeshe upatikanaji wa wawakilishi wa watu wanaoishi na VVU (Me na Ke) kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa kwenye mwongozo huu.
- iii. Afisa Mtendaji wa ngazi husika awezeshe upatikanaji wa mwakilishi wa mtandao/kundi/ shirikisho husika kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa kwenye mwongozo huu.
- iv. Wakaribishwa watakaa katika wadhifa kwa muda wa miaka miwili na miezi sita, akimaliza muda wake anaweza tena kuteuliwa endapo taasisi yake itaona anafaa.

Angalizo: Kila Mtaalam/Mkaribishwa katika kikao cha Kamati atawajibika kutoa taarifa ya utekelezaji wa afua za UKIMWI kutoka katika sehemu au taasisi anayoiwakilisha kila robo mwaka.

3.3 Sifa za Wakaribishwa

Sifa za jumla kwa mjumbe mwalikwa ni kama zifuatazo:

- i. Awe raia wa Tanzania na mkazi wa eneo husika.
- ii. Awe na akili timamu asiyetawaliwa na dutu (substance).
- iii. Ajue kusoma na kuandika.
- iv. Awe na moyo wa kujitolea na utayari wa kuitumikia jamii.
- v. Awe mtu wa mfano wa kuigwa na anayekubalika kwenye jamii.
- vi. Uwakilishi wa vijana uzingatie umri wa kijana unaotambulika kisheria (miaka 18 hadi 35).

3.4 Ukomo wa Ujumbe wa Kamati

Ujumbe wa kamati utakoma iwapo mjumbe:-

- i. Atakosa mojawapo ya sifa zilizotajwa katika sehemu 3.2 ya Mwongozo huu.
- ii. Atafariki.
- iii. Atajiuzulu.
- iv. Atahama eneo la makazi.
- v. Akipatikana na jinai.
- vi. Kukosa kuhudhuria vikao vitatu (3) mfululizo bila kutoa taarifa.
- vii. Atakapokosa sifa za kuwa kwenye Kamati.
- viii. Ikithibitika kukosa uwezo wa kutekeleza wajibu kwenye kamati kwa sababu yoyote ile.

3.5 Ujazaji wa nafasi iliyo wazi

Uchaguzi wa dharura utafanyika kuziba nafasi iliyoachwa wazi kutokana na sababu yo yote kwa kuzingatia utaratibu uliotumika awali kumpata mjumbe.

3.6 Vikao na Agenda za kudumu za Kamati

Kamati itafanya kikao cha kawaida kila baada ya miezi 3. Kikao cha dharura kitaitishwa na Mwenyekiti endapo jambo la dharura na la msingi litajitokeza.

Agenda za kudumu kwenye kikao cha kawaida zitakuwa zifuatazo:-

- i. Taarifa ya hali halisi ya VVU na UKIMWI.
- ii. Taarifa za utekelezaji wa wadau wa afua za VVU na UKIMWI.
- iii. Upatikanaji wa rasilimali za kudhibiti UKIMWI.
- iv. Matumizi ya fedha za kudhibiti VVU na UKIMWI.
- v. Kupokea na kujadili taarifa kutoka ngazi za chini katika Mamlaka husika.
- vi. Hali halisi ya makundi yaliyoko kwenye mazingira hatarishi (WAVIU, Watoto yatima, Watoto Wanaoishi Katika Mazingira Hatarishi, Watu wenye ulemavu, Wajane, Wagane na Makundi Maalum).

3.7 Vigezo vya kupima ufanisi wa Kamati

Ili kuweza kubaini utendaji kazi wa Kamati za kudhibiti UKIMWI Halmashauri itaweka vigezo ambavyo vitajadiliwa katika mkutano wa mwisho wa Mwaka. Vigezo hivyo ni kama vifuatavyo:-

- i. Idadi ya vikao vilivyofanyika.
- ii. Mahudhurio ya wajumbe na wakaribishwa.
- iii. Kiwango cha rasilimali zilizopatikana.
- iv. Utendaji wa Kamati katika ngazi ya chini kwenye Mamlaka husika.
- v. Idadi ya taarifa za utekelezaji zilizowasilishwa ngazi ya juu.
- vi. Matokeo ya maazimio ya Kamati.
- vii. Ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

4.0 UTEUZI WA MRATIBU WA UKIMWI WA HALMASHAURI

Ili kutoa msukumo wa pekee katika kutekeleza na kuratibu afua za UKIMWI, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji atamteua mtaalam maalumu ili kuratibu shughuli za UKIMWI. Mratibu wa UKIMWI wa Halmashauri awe ni Afisa Maendeleo ya Jamii na asiwe Mkuu wa Idara.

4.1 Majukumu ya Mratibu wa UKIMWI wa Halmashauri

Mratibu wa UKIMWI wa Halmashauri atakuwa na majukumu yafuatayo:-

- a) Kuratibu, kupanga na kusimamia shughuli zote za VVU na UKIMWI ngazi ya Wilaya, Mji, Manispaa au Jiji.
- b) Kushirikiana na Mratibu wa UKIMWI Sekta ya Afya katika utekelezaji wa afua za UKIMWI na kukusanya takwimu za UKIMWI katika Halmashauri husika.
- c) Kushirikiana na wadau wa UKIMWI kuandaa mipango ya utekelezaji afua za UKIMWI kupitia zana ya kuandaa Mpango Mkakati wa Mkoa.
- d) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa shughuli za UKIMWI za robo, nusu na mwaka mzima na kuziwasilisha ngazi ya Halmashauri, Mkoa na kwa wadau husika.
- e) Kusimamia na kuratibu shughuli za Waratibu wa UKIMWI na waelimisha rika katika Idara za Halmashauri.
- f) Kubaini mahitaji na kuandaa mpango kazi wa kujenga uwezo miongoni mwa wadau wanaoshughulika na afua za UKIMWI katika Halmashauri.

- g) Kukusanya na kuunganisha taarifa kutoka Kamati za ngazi ya Kata na Mtaa/Vijiji.
- h) Kuwezesha na kuzijengea uwezo Kamati na wadau mbalimbali wa VVU na UKIMWI.
- i) Kufuatilia na kutathimini shughuli za VVU na UKIMWI katika Halmashauri.
- j) Kuandaa kikao cha wadau wa afua za VVU na UKIMWI kila robo mwaka.
- k) Kuwa kiungo kati ya Halmashauri na Umoja wa Mameya na Viongozi wa Miji, Manispaa, na Majiji (AMICAALL). Hii ni kwa Waratibu wa Manispaa na Jiji.
- l) Kufuatilia na kutathimini vichocheo vya maambukizo ya VVU yanayotokana na madawa ya kulevya.

5.0 MAELEKEZO MENGINE YA JUMLA

- (a) Mtiririko wa fedha/nyenzo au rasilimali zingine zitafuata mfumo unaotumika hivi sasa kwenye Halmashauri.
- (b) Halmashauri zitawasilisha mipango ya Kudhibiti UKIMWI iliyopitishwa na Baraza la Madiwani, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania.
- (c) Taarifa za fedha na utekelezaji zitayarishwe kila robo ya mwaka na kuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania. Mtendaji Mkuu katika kila ngazi atawajibika kuratibu na kutoa taarifa za fedha na utekezaji. Mwajibika Mkuu kwa taarifa za eneo lote ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya, Mji, Manispaa au Jiji.
- (d) Halmashauri zitatakiwa kuwa na uwezo na ufanisi zaidi wa kudhibiti UKIMWI katika maeneo yao.
- (e) Serikali haitatoa fedha kwa Halmashauri isiyokuwa na mipango madhubuti ya kudhibiti UKIMWI.

5.0. HITIMISHO

Inasisitizwa kuwa, kupambana na janga la UKIMWI ni miongoni mwa majukumu ya lazima na ya msingi kwa kila Serikali ya Mtaa. Kwa kuwa Halmashauri haziwezi kuwa na amani na utulivu, wala kufanya shughuli za maendeleo endelevu bila Kuudhibiti UKIMWI, janga hilo halina budi kupigwa vita kwa nguvu na uwezo wote. Ni mategemeo ya OWM-TAMISEMI kuwa mtatekeleza jukumu hili kwa bidii na umakini unaostahili.



Jumanne A. Sagini
KATIBU MKUU
OWM-TAMISEMI